





Nozibele na nywele tatu





-  Tessa Welch
 - Wiehan de Jager
 -  Matteo E. Mwita
- || 3
-  Kiswahili! SW



Global Storybooks

globalstorybooks.net


Nozibele na nywele tatu

-  Tessa Welch
- Wiehan de Jager
-  Matteo E. Mwita




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>







Hapo zamani za kale, wasichana
watatu walienda kukusanya kuni.



Ilikuwa ni siku yenye jua kali na
wakaamua kwenda mtoni kuogelea.
Wakaogelea huku wakicheza na
kursuhiana maji.




Mbwa akagundua kuwa Nozibele
amemkimbia. Kwa hiyo akakimbia
kuelekea kijijini. Kaka zake Nozibele
walikuwa wakimsubiri na fimbo.
Mbwa alipowaona akageuka na
kukimbia, na hajawahi kuonekana
tena.




Ghafla waligundua kuwa muda umekwenda. Wakaharakisha kurudi nyumbani.




Mbwa aliporudi akaanza kumtafuta Nozibele. "Nozibele, uko wapi?" akapiga kelele. "Niko hapa, chini ya kitanda," unywele wa kwanza ukajibu. "Nipo hapa nyuma ya mlango," unywele wa pili ukajibu. "Niko hapa kwenye uzio," unywele wa tatu ukajibu.



Walipokuwa wanakaribia kufika
nyumbani, Nozibele akajishika
shingoni. Alikuwa amesahau shanga
zake! "Tafadhali turudini!" aliwasihi
rafiki zake. Lakini rafiki zake
wakasema tumechelewa.




Mara baada tu ya mbwa kuondoka,
Nozibele akanyofoa nywele tatu
kutoka kwenye kichwa chake.
Akaweka unywele mmoja chini ya
kitanda, mmoja nyuma ya mlango,
na mwingine akaweka kwenye uzio
wa nyumba. Halafu, akakimbia
kuelekea nyumbani kwa nguvu zote.




Kwa hiyo Nozibele akarudi mwenyewe mtoni. Akapata shanga zake na akakimbia kurudi nyumbani. Lakini akapotea gizani.




Akawa kila siku anampikia, anamfulia na kumfagilia mbwa. Siku moja mbwa akasema, "Nozibele, leo naenda kuwatembelea rafiki zangu. Fagia nyumba, pika chakula na osha vitu vyangu kabla sijarudi."



kwa mbali akaona mwanga unatoka
kwenye nyumba. Akakimbia
kwenye nyumba na kugonga
mlango.



Mbwa akamwambia, "Nitandikie
kitanda!" Nozibele akajibu, "Sijawahi
kumtandikia mbwa kitanda."
"Tandika kitanda, la siyo
nitakung'atai" mbwa akasema.
Nozibele akatandika kitanda.



Akastaajabu kumwona mbwa akifungua mlango na akasema, “Unataka nini?” “Nimepotea na ninatafuta sehemu ya kulala,” akasema Nozibele. “Ingia ndani, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akamwambia. Nozibele akaingia ndani.



Mbwa akamwambia, “Nipikie!” “Sijawahi kumpikia mbwa,” akajibu. “Pika, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akasema. Nozibele akampikia mbwa chakula.